# MZOZO WA UTAMBULISHO WA MAMLAKA MAKUU: MBINU YA KUONDOA UKOLONI KATIKA TEKNOLOJIA DIJITALI INAONYESHA NINI KUHUSU MZOZO WA UTAMBULISHO WA MAMLAKA MAKUU?

*Nanjala Nyabola*

Dhana ya "mzozo wa utambulisho wa mamlaka makuu" katika enzi ya dijitali ina dhana nyingi zinazobishwa - mamlaka makuu, utambulisho na hata enzi ya dijitali.[1] Hata hivyo, ni dhahiri kwamba mzozo wa aina fulani unaounganisha masuala haya yote unaendelea. Huluki inayochukuliwa kumiliki mamlaka makuu - yaani nchi - inapingwa kwa njia mbalimbali kama vile ukinzani, mizozo na uhamaji wa watu wengi; mengi ya hayo yanaratibiwa au kukuzwa na teknolojia dijitali. Msukumo wa kuitaka mifumo ya kimataifa isuluhishe mizozo kati ya mataifa kuhusu masuala ya teknolojia dijitali yakiwemo utozaji kodi, utengenezaji, uzalendo na mengineyo, unazidi kuenea. Aina zote za utambulisho hufanywa kupitia mifumo dijitali ya utambulisho, iwe ni uraia au utambulisho wa kijinsia au wa kikabila. Bila shaka mabadiliko makubwa yanafanyika na kazi iliyopo ni kufafanua mzozo huo kwa njia inayoangazia mpango mwafaka wa hatua za kuchukuliwa na kuwapigisha wanadamu hatua mbele.

Kimsingi, ahadi ya enzi ya dijitali ilikuwa kwamba kwa kuboresha usafiri na mawasiliano, tungeweza kuwaleta watu binafsi na pia jamii karibu zaidi. Badala yake, karne ya 21 inaonekana kuwa kipindi cha kugawanyika kwingi, kinyume na ishara za maendeleo ambazo pia zinadhihirika katika kila ngazi ya jamii. Watu, jamii na mifumo zaidi sasa imeunganishwa kushinda hapo zamani, lakini kwa wengi, hali yao ya matumizi ya dijitali imegawanyika. Kwa mfano, idadi kubwa ya watu duniani hutumia intaneti kupitia tafsiri au kidhahania kwa sababu intaneti inachukulia kwamba mtumiaji wa kawaida ni mwanamume anayezungumza Kiingereza, mwenye elimu nzuri na ambaye ana nguvu nyingi sana za kisiasa nje ya mtandao kiasi kwamba kubanwa kwa haki zake dijitali mtandaoni ni ukiukaji mdogo tu wa muktadha wa haki zake kijumla. Hili linadhihirika katika idadi kubwa ya teknolojia dijitali ambazo zinapatikana kwa Kiingereza pekee, jinsi haki za wanawake zinavyodunishwa mtandaoni kila uchao na jinsi kampuni kuu za teknolojia zinavyokosa kupatia kipaumbele njia zinazozingatia haki za kubuni teknolojia. Couldry na Mejias (2019) wanaeleza kwamba uchopoaji wa malighafi ndio kiini cha mfumo wa sasa wa kubuni na kuendeleza teknolojia na kwamba hili linasadikisha madai ya ukoloni dijitali. Kimsingi, lengo la ukoloni lilikuwa kubadilisha sehemu fulani za ulimwengu na watu walioishi au kutokea huko kuwa maeneo ya kuchopoa malighafi kwa manufaa ya maeneo mengine ya ulimwengu. Si

1. Imetayarishwa kutokana na Hotuba Kuu ya Kongamano Iliyotolewa 17 Novemba 2022. Baadhi ya mawazo yaliyowasilishwa katika makala hii yanapatikana katika Nanjala Nyabola. *Digital Identities and Border Cultures: The Limits of Technosolutionism in the Management of Human Mobility [Utambulisho Dijitali na Tamaduni za Mipakani: Upungufu wa Utatuzi Teknolojia katika Udhibiti wa Uhamiaji wa Watu]*, Washington DC, Atlantic Council, 2023

suala la utwaaji wa data tu, bali ni utwaaji wa data "kwa masharti ambayo kwa kiasi fulani au kabisa hayawezi kudhibitiwa na mtu ambaye data hiyo inamhusu".[2]

Kwa hivyo, makala hii inatoa hoja kwamba mfumo bora zaidi wa kinadharia wa kukabiliana na mzozo wa mamlaka makuu, bila kuzidisha utenganisho ambao tayari unaletwa na enzi ya dijitali katika maeneo mengi duniani, ni mfumo wa kuondoa ukoloni. Ikiangazia zaidi ya dhana pungufu kuhusu mamlaka makuu zisizotambua vya kutosha tofauti za nguvu kati ya wahusika mbalimbali wa data katika jamii tofauti, makala hii inachunguza eneo ambapo tofauti za nguvu ni kubwa zaidi na dhahiri zaidi - mpakani. Makala hii inatoa hoja kwamba siasa za kijela za mipaka ni dalili ya matumizi yaliyokithiri ya mamlaka makuu dhidi ya vikundi vilivyo hatarini sana, na pia zinapelekea mgongano kati ya nchi zinazotumia siasa hizo na dhana zilizokita za hali ya kuwa nchi na ushirikiano wa kimataifa. Hivyo, kwa kutumia mpaka kama mfano na pia eneo muhimu katika kuelewa mzozo wa mamlaka makuu, makala hii inatoa hoja kwamba mbinu ya kuondoa ukoloni katika kuelewa teknolojia dijitali inahitajika katika kukabiliana na madhara yaliyopo na yajayo kutokana na mzozo huo.

## KUBAINISHA UPEO

Ni muhimu kubainisha mwanzoni kwamba ukoloni si tamathali. Kimsingi, kuwa chini ya ukoloni ni kupoteza mamlaka makuu ya nchi yako na yako mwenyewe kwa manufaa ya kiuchumi na ya kijamii ya jamii nyingine - kutekeleza ukoloni ni kulazimisha mamlaka makuu ya upande mmoja juu ya mamlaka makuu ya mwingine. Mchakato wa kuendeleza ukoloni kusini mwa dunia bado ungalipo leo katika hali ya kuchelewa kuachia huru maeneo kama vile visiwa vya Chagos au Martinique[3]. Aidha, ukatili na athari za ukoloni bado zinadhihirika si tu kwa jinsi mataifa yaliyotawaliwa na wakoloni yanavyozidi kunyonywa kwa kile Kwame Nkrumah alichokiita "ukoloni mamboleo"[4], bali pia kwa makovu ya vizazi katika wazawa wa waliotawaliwa na wakoloni katika lugha, uhamiaji wa watu wengi na mengineyo[5]. Hivyo basi, kuondoa ukoloni ni mchakato wa kuondoa desturi ya ukoloni katika jinsi watu binafsi wanavyouona ulimwengu na kuishi humo, katika mpangilio wa jamii mbalimbali, pamoja na kushughulikia madhara yaliyosababishwa na ukatili wa ukoloni.

2. Couldry, Nick na Ulises Ali Mejias. *The Costs of Connection: How Data Is Colonizing Human Life and Appropriating It for Capitalism [Gharama ya Kuunganishwa: Jinsi Data Inavyotawala Maisha ya Watu na Kuyanyakua kwa ajili ya Ubepari]*, Culture and Economic Life [Utamaduni na Maisha ya Kiuchumi], Stanford University Press, 2019., p 5.

3. Boffey, Daniel na Daniel Boffey, Mwandishi Mkuu wa Habari. 'Negotiations on Chagos Islands' Sovereignty Face Legal Challenge' ['Majadiliano kuhusu Uhuru wa Visiwa vya Chagos Yapingwa Kisheria'], *The Guardian*, 9 Januari 2023, sehemu ya World news [habari za kimataifa], https://www.theguardian.com/world/2023/jan/09/negotiations-chagos-islands-sovereignty-legal-challenge-talks-uk-mauritius [https://perma.cc/F2ZB-3WNR].

4. Nkrumah, Kwame. *Neo-Colonialism: The Last Stage of Imperialism [Ukoloni Mamboleo: Hatua ya Mwisho ya Ubeberu]*, 6. kimechapishwa. New World Paperbacks 140. New York: International Publ., 1976.

5. Angalia Nyabola, Nanjala. 'Uraia, Lugha Na Haki Za Kidijitali: Umuhimu Wa Lugha Katika Harakati Za Kuondoa Ukoloni Katika Teknolojia'. *Foresight*, 13 Oktoba 2022. https://doi.org/10.1108/FS-11-2021-0222.

Frantz Fanon, msomi mtajika wa uondoaji wa ukoloni, alisisitiza kwamba kuondoa ukoloni ni mchakato wa kuvuruga kwa asili yake[6]. Kutumia uondoaji wa ukoloni kama mbinu pia ni njia inayovuruga kwa sababu inajumuisha matumizi ya nyenzo ambazo huenda hazifahamiki vizuri au hazihimizwi katika usomi wa kawaida. Kwa mfano, inamaanisha kufanya kazi inayohusisha tofauti za lugha na utamaduni, na hivyo kujumuisha michakato kama vile tafsiri au unukuzi ambayo misingi yake imo katika miktadha isiyofahamika na wengi. Kwa mtafiti, inaweza kumaanisha kufanya kazi katika kiwango cha chini cha kidhahania kinachotuwezesha kuunganisha michango ya fani zinazoonekana tofauti sana. Inamaanisha kurahisisha maswali ili yaweze kueleweka au kunyumbuliwa katika taaluma mbalimbali. Katika kazi yangu ya utafiti, ninafafanua kwamba ili kuondoa ukoloni kabisa kwenye intaneti ni sharti tuanze na mfumo tofauti wa marejeleo na tuanze na mhusika mkuu tofauti wa kurejelewa. Hivyo, kwa minajili ya uchambuzi huu, mbinu ya kuondoa ukoloni inachanganua suala la mzozo wa mamlaka makuu kwa maswali mepesi ya maana ya nchi kuwa na mamlaka makuu na jinsi ya kubuni upya dhana ya mamlaka makuu kwa njia isiyoongeza madhara.

Sehemu kubwa ya ninachoshiriki nanyi leo inatokana na minyororo miwili ya utafiti ambao nimekuwa nikiufanya katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita. Mnyororo wa kwanza ni utafiti kuhusu uondoaji wa ukoloni na Intaneti huku nikijaribu kuhoji mifumo ya mamlaka dhahiri na isiyo dhahiri inayobaini jinsi tunavyotumia intaneti. Mnyororo wa pili unahusu wakimbizi na uhamiaji. Minyororo yote miwili ipo akilini mwangu, kwa sababu mipaka na hususan wakimbizi, wanazidi kuathiriwa na kukithiri kwa ufuatiliaji dijitali na tabia za kijela za nchi. Hata hivyo, kwa sababu wakimbizi huwa mbali na mamlaka ya nchi walizotoroka, kuna uwezekano mdogo wa wanaoathiriwa na matumizi ya mamlaka makuu kupita kiasi mpakani kulalamika kuhusu hali hiyo. Hili linadhihirika katika vifo vya wengi katika mipaka inayozidi kutumia teknolojia dijitali na kulindwa na katika maeneo yanayoizunguka katika nchi jirani - katika Bahari ya Kati, katika Eneo la Darien na mpaka wa Meksiko au yanayoizunguka Somalia, Afrika Mashariki.

Mipaka ya kisasa inaonyesha nini kuhusu dhana ya mamlaka makuu katika enzi ya dijitali? Labda njia rahisi ya kujibu swali hili ni kuanza na muundo msingi wa mamlaka makuu. Hobbes, Rousseau, Locke na wengine wanatoa wazo la msingi kwamba watu hutoa baadhi ya haki zao kwa huliki ambayo sasa hupata mamlaka ya kutawala, kuratibu uhusiano wetu mmoja kwa mwingine na pia uhusiano wetu na huluki yenyewe[7]. Huwa tunafanya hivi kwa sababu tunaamini kwamba kimsingi, tutafaidika zaidi ndani ya mfumo wenye mpangilio kuliko nje ya mfumo kama huo. Nje ya mfumo huo kuna uwezekano mkubwa kwamba tutazozana bila ustaarabu kwa njia mbalimbali, lakini ndani ya mfumo, tunaweka uthabiti unaotuwezesha kushughulikia maazimio au miradi ya kiwango cha pili. Kwa hivyo, katika mpangilio huu, mwenye mamlaka makuu ni

6. Fanon, Frantz na Jean-Paul Sartre. *The Wretched of the Earth [Walalahoi wa Dunia]*, Kimetafsiriwa na Constance Farrington. Kimechapishwa Tena. Penguin Classics. London New York: Penguin Books, 2001., uk 27.

7. Angalia kwa jumla, LOCKE, JOHN, *SECOND TREATISE OF GOVERNMENT [TASNIFU YA PILI KUHUSU SERIKALI]*, Mahali kilipochapishwa hapajabainishwa: SMK Books, 2018; Angalia pia Hobbes, Thomas na Christopher Brooke. *Leviathan*. Penguin Classics. Harmondsworth, Meddlesex: Penguin Books, 2017.

huluki ambayo watu hukabidhi sehemu ya haki zao kama watu binafsi kwa masilahi ya wote. Huu ndio mkataba wa kijamii.

Aina ya mwenye mamlaka makuu hutofautiana katika jamii mbalimbali, kuanzia wafalme, marais, mabunge, mabaraza ya kisiasa na nyinginezo. Mifumo hii yote inaunganishwa na wazo kwamba mamlaka makuu ni sifa ya asili ya nchi, au angalau, ya huluki ya kisiasa inayoweza kudai kuwakilisha zaidi ya mtu mmoja. Mamlaka makuu ni zaidi ya mfumo wake - yamkini yanabainishwa zaidi na uwezo na upeo wake wa kutenda. Kwa kweli, funzo moja muhimu kutoka nchi zilizotawaliwa na wakoloni ni kwamba kuzingatia aina ya mwenye mamlaka makuu zaidi ya vitendo vyake kunaweza kuficha mahali nguvu halisi zilipo katika jamii. Kwa mfano, kusisitiza sana uchaguzi wa urais, badala ya mitandao isiyo rasmi ya nguvu za kisiasa inayoelekeza matokeo ya kisiasa katika jamii, kunaweza kuficha mahali mamlaka makuu yanapatikana. Huenda dhana ya mamlaka makuu ikafaidi kuliko ile ya mwenye mamlaka makuu. Mamlaka makuu ni sifa msingi ya mwenye mamlaka makuu inayompatia nguvu za kuratibu mahusiano ya kijamii, kisiasa na ya kiuchumi katika kikundi cha kisiasa. Mamlaka makuu ni sifa na dhihirisho la nguvu.

Mbali na mapokeo ya falsafa ya Magharibi, kunazo nadharia nyingi ambazo zinaweza kuelekeza kuwazia mamlaka makuu kwa njia hii pana. Katika falsafa ya Kiislamu, Mkataba wa Madina wa mwaka 622, kiongozi anapochukua mamlaka makuu, mamlaka yake yanatokana na wajibu wake wa kuwa mwadilifu. Kuwa na mamlaka makuu hutokana na ubayana wa maadili[8]. Hii inalingana na dhana ya mamlaka ya mbingu iliyosisitizwa na Confucius, ambayo inatoa hoja kwamba mtawala ana wajibu wa kufanya kazi kuendeleza maslahi ya kiuchumi ya watu wanaotawaliwa kwa mamlaka makuu[9]. Hoja inayounganisha mitazamo hii yote ni kwamba mamlaka makuu hutokana na idhini ya kisiasa. Ambapo mamlaka makuu ndiyo mamlaka ya juu zaidi ya nchi yanayovikwa kiongozi wa nchi hiyo, mamlaka hayo hutolewa kwa kiongozi huyo kwa idhini, na yanaweza kuondolewa kiongozi huyo anapotenda kinyume na maslahi ya kiuchumi na ya kijumuiya ya wanaotawaliwa. Hivyo, dhana za mamlaka makuu na mahali mamlaka hayo yanapatikana zinavyozidi kubishwa na kubainishwa upya, mabadiliko yanayosababishwa na enzi ya dijitali yanabadilishaje mawazo kuhusu maana ya kuwa na mamlaka makuu?

Katika usomi wa kisheria, dhana ya nchi mara nyingi huwasilishwa kama jambo thabiti, lakini sivyo katika hali halisi. Je, nchi ni huluki au ni asasi? Nchi i wapi? Mwanasosholojia wa Ufaransa Pierre Bourdieu anaeleza kwamba nchi si asasi vile bali ni mtandao wa mahusiano yanayobadilika kila wakati, na ambamo aina tofauti za nguvu

---

8. Angalia Dabashi, Hamid. *Authority in Islam: From the Rise of Mohammad to the Establishment of the Umayyads [Mamlaka katika Uislamu: Kuanzia Kuinuka kwa Muhammad hadi Kuasisiwa kwa Wamuawiya]*, Toleo la Kwanza. London: Taylor na Francis, 2017., Angalia pia Yildirim, Yetkin. 'The Medina Charter: A Historical Case of Conflict Resolution' ['Mkataba wa Madina: Mfano wa Kihistoria wa Utatuzi wa Migogoro'], *Islam and Christian–Muslim Relations* 20, nambari. 4 (2009): 439–50. https://doi.org/10.1080/09596410903194894.

9. Angalia kwa jumla Jiang, Yonglin. *The Mandate of Heaven and the Great Ming Code [Mamlaka ya Mbingu na Kanuni za Utawala wa Nasaba ya Ming]*, Asian Law Series [Mfululizo kuhusu Sheria za Asia], nambari. 21. University of Washington Press, 201.

na rasilimali huingiliana ili kuleta matokeo fulani[10]. Hivyo basi nchi si asasi tu, bali pia ni desturi za asasi hizo. Nchi huzalisha na ni zao la mahusiano baina ya asasi mbalimbali zilizopo katika eneo fulani la kijiografia. Kuwaza kwa njia hii kuhusu nchi kunatusaidia kupanua mawazo au mtazamo wetu kuhusu mahali nchi hutekeleza vitendo vyake.

Kwa hivyo, dhana ya mamlaka makuu si himaya ya serikali ya kitaifa pekee. Kwa mfano, katika mahusiano ya kimataifa, ukuaji wa asasi za kieneo umekaidi dhana kwamba mamlaka makuu yapo tu katika serikali ya kitaifa. Barani Ulaya kwa mfano, Umoja wa Ulaya ni huluki iliyo juu ya mataifa ambayo inaleta aina mpya ya mamlaka makuu yasiyoweza kubainishwa kwa mipaka ya kitaifa tu. Idara ya mipakani ya Ulaya, FRONTEX, imebuni siasa na mtazamo wayo kuhusu masuala ya mipakani, ambao wakati mwingine hautilii maanani ajenda za siasa za kitaifa[11]. FRONTEX inapobuni masharti kuhusu matumizi ya Akili Unde katika udhibiti wa mipaka ambayo yamepita upeo wa desturi za kitaifa za nchi wanachama wa Umoja wa Ulaya, inaratibu mahusiano ya kijamii, ya kisiasa na ya kiuchumi. Inaamua wanaostahili kuwa huko na wasiostahili kuwa huko, wanaoweza kufanya kazi huko na wasioweza kufanya kazi huko; hiki ni kitendo cha mamlaka makuu kwa niaba ya Umoja wa Ulaya, wala si kwa niaba ya nchi moja moja ambazo ni wanachama.

## MAMLAKA MAKUU MPAKANI

Huenda mpakani ndipo eneo kuu ambapo mamlaka makuu yanadhihirishwa katika enzi ya kisasa. Kuwa na mamlaka makuu ina maana kwamba mahusiano yanayotawala nyanja za kisiasa, kijamii na kiuchumi katika jamii fulani yanafanya kazi bila ushawishi au maagizo ya huluki zilizo nje ya mfumo wa mahusiano yanayoingiliana katika jamii hiyo. Hivyo, hata nchi zinazoainishwa kama nchi zilizofeli katika orodha ya shirika la Freedom House, kwa kawaida zitaweka taratibu kabambe za ulinzi mipakani kwa madhumuni ya kubainisha wenyeji na hivyo kuwatenga watu wa nje, kuchota mapato kutoka kwa wanaoruhusiwa kuingia au kuonyesha nguvu kwa majirani na nchi adui. Ruben Zaiotti, msomi wa siasa za mpakani za Ulaya, anatumia istilahi “tamaduni za mipakani” kufafanua jinsi mahusiano na mwingiliano wa nguvu kati ya wahusika mbalimbali, hasa Ulaya, zinavyoibua masuala mapya ya mamlaka makuu mipakani[12]. Tamaduni za mipakani hazitokani na siasa za kitaifa tu, bali pia zinatokana na mwingiliano wa nguvu kati ya nchi tofauti katika muungano, vyama tofauti vya kisiasa na ushirika wanaoufanya baina yao, na hata siasa pinzani au tamaduni pinzani zinazopinga vikundi hivi.

10. Bourdieu, Pierre. *On the State: Lectures at the Collège de France [Kuhusu Nchi: Mihadhara katika Chuo cha Collège de France]*, *1989 - 1992*. Kimehaririwa na Patrick Champagne, Remi Lenoir, Franck Poupeau na Marie-Christine Rivière. Kimetafsiriwa na David Fernbach. Cambridge Malden, MA: Polity, 2014., u.k. 11.

11. Statewatch, ‘EU Has Spent over €340 Million on Border AI Technology That New Law Fails to Regulate’ [‘Umoja wa Ulaya umetumia zaidi ya Yuro Milioni 340 kwa Teknolojia ya Akili Unde Mipakani Ambayo Haidhibitiwi na Sheria Mpya’], Ilifunguliwa 20 Februari 2023. https://www.statewatch.org/news/2022/may/eu-has-spent-over-340-million-on-border-ai-technology-that-new-law-fails-to-regulate/ [https://perma.cc/RPJ8-LN52].

12. Zaiotti, Ruben. ‘Cultures of Border Control: Schengen and the Evolution of European Frontiers’ [‘Tamaduni za Udhibiti wa Mipaka: Schengen na Mageuko katika Mipaka ya Ulaya], University of Chicago Press, 2011.

Ujio wa enzi ya dijitali umechangia pakubwa kuibuka kwa tamaduni mpya za mipakani, hasa zile zenye misingi ya kijela[13] au mantiki ya kutia gerezani, kuonyesha nguvu nje ya nchi au kutandisha mpaka katika maeneo jirani. Mengi ya haya yanawezeshwa na teknolojia dijitali. Teknolojia ya ufuatiliaji ni sehemu msingi ya desturi za kijela mipakani, huku mifumo ya bayometriki na ya utambulisho dijitali ikiwezesha mipaka kumfuata mtu popote alipo nchini. Mabadiliko haya bila shaka yanakinzana na mtazamo wa kitamaduni kwamba mpaka ndio upeo wa baadhi ya nguvu za nchi, hasa nguvu za nchi ng'ambo. Hata hivyo, kwa mfano, uwezo wa serikali za Magharibi kutaka ushahidi wa viza na usafiri wa kurudi kutoka kwa wasafiri Waafrika katika nyaja za ndege barani Afrika kabla ya wasafiri kuruhusiwa kuabiri ndege, ni kutanda kwa mpaka wa Magharibi katika siasa za Afrika. Mwitiko wa serikali na wananchi kuzoelea mabadiliko haya na mengine ni sehemu ya mzozo mpana wa mamlaka makuu unaokabili nchi ya sasa.

Hivi leo, pasipoti si hati inayopigwa muhuri mpakani tu. Pia ni data inayozalishwa na kusambazwa katika asasi mbalimbali katika eneo la kitaifa na la kimataifa. Kwa mfano, katika nchi kama vile Marekani, rekodi za kuhudhuria masomo za wanafunzi wa kigeni mara nyingi hutumika kama sehemu ya shughuli pana za kufuatilia na kudhibiti vikundi hivi[14]. Tishio la kuondolewa mara moja nchini huwafuata wanafunzi wa kigeni hadi darasani, na wahadhiri na wafanyakazi wa vyuo huingizwa katika shughuli ya kulinda mipaka hii.

Hata hivyo, dhana ya Marx ya "ashiki iliyokithiri" ni muhimu katika kuelewa kwa nini teknolojia dijitali zina mvuto mkubwa kwa serikali zinazotaka kudhihirisha mamlaka makuu mpakani. Marx anatukumbusha kwamba thamani ya vitu mara nyingi inazidi thamani halisi inayotumika kuvitengeneza au kuvitumia, pia inahusiana na thamani ambayo watu wanaovitumia wanavipatia[15]. Kwa kiasi fulani, manufaa *yanayodhaniwa* ya teknolojia dijitali katika kuboresha tamaduni za mpakani yanazidi manafuu halisi yanayopatikana. Kwa mfano, FRONTEX na mamlaka mengine ya mipakani yanatetea wazo kwamba Akili Unde inaweza kuimarisha sana ulinzi wa mipaka Ulaya,[16] ilhali utafiti mwingi umeonyesha mapungufu makubwa ya Akili Unde katika

---

13. Angalia kwa jumla LeBaron, Genevieve na Adrienne Roberts. 'Toward a Feminist Political Economy of Capitalism and Carcerality' ['Kuelekea Uchumi wa Kisiasa wa Kifeministi wa Ubepari na Desturi za Kijela'], *Signs: Journal of Women in Culture and Society [Signs: Jarida la Wanawake katika Utamaduni na Jamii]* 36, nambari. 1 (2010): 19–44. https://doi.org/10.1086/652915.

14. Allen, Ryan na Krishna Bista, 'Talented, Yet Seen with Suspicion: Surveillance of International Students and Scholars in the United States' ['Wana Vipaji, Lakini Wanatiliwa Shaka: Ufuatiliaji wa Wanafunzi na Wasomi wa Kigeni nchini Marekani'], *Journal of International Students [Jarida la Wanafunzi wa Kigeni]* 12, nambari. 1 (9 Julai 2021), https://doi.org/10.32674/jis.v12i1.3410.

15. Angalia Hornborg, Alf. 'Technology as Fetish: Marx, Latour, and the Cultural Foundations of Capitalism' [Teknolojia kama Ashiki Iliyokithiri: Marx, Latour na Misingi ya Kitamaduni ya Ubepari'], *Theory, Culture & Society [Nadharia, Utamaduni na Jamii]*, 31, nambari. 4 (2014): 119–40. https://doi.org/10.1177/0263276413488960.

16. 'Artificial Intelligence - Based Capabilities for European Border and Coast Guard' ['Nyenzo za Akili Unde kwa ajili ya Mamlaka za Mipaka na Kulinda Pwani Barani Ulaya] - Ilifunguliwa 20 Februari 2023, https://frontex.europa.eu/media-centre/news/news-release/artificial-intelligence-based-capabilities-for-european-border-and-coast-guard-1Dczge [https://perma.cc/RP7D-GLZF]; Angalia pia *Frontex publishes technology foresight on biometrics for the future of travel [Frontex yachapisha utabiri wa teknolojia kuhusu bayometriki katika usafari wa siku zijazo]* (n.d.), Ilifunguliwa 3 Desemba 2022, kutoka,

muktadha huu, hasa kwa jinsi inavyoweka mfumo wa ubaguzi na dhuluma dhidi ya vikundi mahususi ambavyo tayari vinalengwa na ubaguzi uliokita katika siasa za mpakani Ulaya[17].

Mpaka si kitu halisi. Mpaka unawakilisha makubaliano dhaifu kuhusu masuala msingi ya kisiasa na mizozo. Kati enzi zilizotangulia enzi ya kisasa, mipaka kati ya jamii mbalimbali ilikuwa nyumbufu na ilitegemea hali ya mahusiano kati ya jamii zilizojiona kuwa tofauti. Mara nyingi mipaka ililingana kijuujuu na sura ya nchi kama vile mito au milima lakini iliweza kubadilishwa kwa urahisi na uvamizi au uhamiaji. Barani Ulaya, Mkataba wa Westphalia wa mwaka 1648 mara nyingi hurejelewa kama wakati ambapo mipaka mingi ya Ulaya iliamuliwa na mara nyingi hutajwa kama asili ya nchi ya kisasa. Westphalia hutajwa kama mfano bora zaidi wa kwa nini mipaka ni maendeleo mema ya kisiasa ukizingatia historia ndefu ya mizozo ya mipaka katika bara hilo.[18]

Kwa jumla, inatambulika kwamba mzozo wa mamlaka makuu unaendelea na kwamba mpaka ni eneo muhimu la mzozo huu, lakini nchi nyingi zinakosa kutambua mahali hasa mzozo huu ulipo. Badala ya kuona mzozo huu kama mkinzano kati ya dhana ya zamani ya haki na majukumu ya mwenye mamlaka makuu na maonyesho ya nguvu yanayowezeshwa na ujio wa dijitali, nchi nyingi zinashikilia kwamba mzozo ulio mpakani upo katika idadi kubwa ya watu kutoka Kusini mwa dunia wanaojitayarisha kuhamia Kaskazini. Takwimu zinaashiria kwamba hilo si kweli hata kidogo. Kwa mujibu wa Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (IOM), kati ya mwaka wa 1970 na 2020, jumla ya idadi ya wahamiaji iliongezeka kutoka asilimia 2.3 ya watu duniani hadi asilimia 3.6 ya sasa.[19] Upotoshaji huu wa mahali hasa mzozo unapofanyika unachochea matakwa ya mbinu changamano zaidi za ulinzi na udhibiti mipakani.

## MAHALI HASA MZOZO ULIPO

Kwa pamoja, wanadamu hivi leo wamestawi zaidi ya wakati mwingine wowote katika historia. Lakini kuna mzozo wa haki katika ugavi; changamoto kubwa zaidi iliyopo katika suala la rasilimali katika ulimwengu wa sasa si upatikanaji bali ni ukosefu wa usawa. Bila shaka, kila mtu aliyehamishwa anawakilisha mzozo wa aina fulani, lakini kama asilimia ya watu wote duniani, idadi ya wahamiaji haijabadilika sana. Cha muhimu ni kwamba sehemu ya wahamiaji duniani wanaoondoka eneo lao la asili imesalia kuwa chini. Katika Ripoti ya Uhamiaji Afrika ya mwaka wa 2020, ambayo nilikuwa mmoja wa wahariri, tulijaribu kuonyesha baadhi ya migogoro inayotokana na kukubali, bila kuhoji, wazo kwamba kila mzozo katika udhibiti wa mipaka unatokana na ongezeko

https://frontex.europa.eu/future-of-border-control/eu-research/news-and-events/frontex-publishes-technology-foresight-on-biometrics-for-the-future-of-travel-us6C6v [https://perma.cc/6VWX-TW7K].

17. Zuiderveen Borgesius, F. 'Discrimination, Artificial Intelligence, and Algorithmic Decision-Making' ['Ubaguzi, Akili Unde na Uamuzi wa Alogaridhimu'], 2018; Angalia pia Noble, Safiya Umoja, *Algorithms of Oppression: How Search Engines Reinforce Racism [Alogaridhimu za Dhuluma: Jinsi Mitambo ya Kutafuta Inavyokuza Ubaguzi wa Rangi]*, New York University Press, 2018.

18. Stephen Okhonmina, "States without Borders: Westphalia Territoriality under Threat" ["Nchi zisizo Mipaka: Tishio kwa Mtazamo wa Westphalia wa Kugandamia Maeneo"], *Journal of Social Sciences [Jarida la Sayansi Jamii]* 24, nambari. 3 (2010): 177–82, https://doi.org/10.1080/09718923.2010.11892853.

19. McAuliffe na Triandafyllidou, *World Migration Report 2022 [Ripoti ya Uhamiaji Duniani 2022].*

halisi la idadi ya wahamiaji.[20] Ripoti hiyo ilisisitiza ukweli kwamba watu wengi wanaohama hawaondoki katika nchi au eneo lao la asili - yaani, hawakabili mamlaka makuu ya nchi mpakani. IOM inarekodi wahamiaji milioni ishirini na tano Afrika, lakini wengi wa wanaobadilisha nchi yao ya asili Afrika hubaki katika eneo lao au katika nchi yao ya asili.[21] Ni vyema kutambua kwamba isipokuwa Ujerumani, ambayo ina wakimbizi milioni 1.2 na imefuata sera ya kuwakaribisha zaidi ikilinganishwa na nchi nyingine za Umoja wa Ulaya, makundi makubwa zaidi ya wakimbizi duniani hayapatikani Ulaya Magharibi wala Amerika ya Kaskazini. Katika mwaka 2022, Uturuki imekuwa mwenyeji wa idadi kubwa zaidi ya wakimbizi, watu milioni 3.7, ikifuatwa na Colombia, Uganda na Pakistan, kila moja ikiwa na chini ya nusu ya idadi hiyo.[22] Ambacho kimebadilika si *idadi inayowiana* ya watu wanaohama, bali ni *nia* ya kuzuia matukio au vigezo vinavyosababisha uhamiaji wa watu na kuwakimu wanapohama.

Aidha, ingawa dhiki ya tabianchi mara nyingi hutajwa kusababisha ongezeko kubwa la wakimbizi Kaskazini mwa Dunia, hili pia linaonyesha hamu ya kufafanua changamoto za pamoja kwa njia fulani ili kukusanya rasilimali za kuzikabili. Yaani, inaonyesha kwamba tishio la mabadiliko ya tabianchi limebadilishwa kuwa suala la usalama. Hakika mabadiliko ya tabianchi yanasababisha kuhamishwa kwa watu wengi, lakini ni muhimu kukumbuka kwamba mabadiliko ya tabianchi ni tisho la uhai wote na si la mahali fulani. Hatari ya mabadiliko ya tabianchi haiwezi kukabiliwa kwa kuongeza vizuizi mipakani au tamaduni za kijela mipakani: kinyume na hayo, inahitaji kuvunjwa kwa mitazamo finyu na pawe na jitihada za kimataifa, na zinazozidi nchi kwa kweli.

Hali ya nchi kupendelea na kustahimili mtazamo wa kueneza hofu kuhusiana na data ya uhamiaji inadokeza kwamba mzozo wa mamlaka makuu unatokea kwingineko. Mtazamo huu wa kueneza hofu kuhusiana na data ya uhamiaji hutumika kama kisingizio cha kuwakandamiza vikali wakimbizi na wahamiaji katika maeneo fulani duniani, hususan kwa sababu serikali za nchi hizo zinashindwa kukabiliana na changamoto kubwa za kindani. Serikali, hasa zenye shauku ya kuonekana imara huku zikikabiliwa na masuala changamano ya kijamii na kufanana kwa sera za kiuchumi, hujitahidi kujitofautisha na nyingine kwa kuleta siasa katika suala la uhamiaji. Ni fursa ya kusisitiza mamlaka makuu.

Hali ya sera nyingi kuzingatia hoja kuhusu uhamiaji za vyama vyenye msimamo mkali wa mrengo wa kulia katika mataifa mengi ya Magharibi, ikithibitishwa na ukweli kwamba hata vyama vya maendeleo kwa jina tu duniani kote vinazidi kurudia mapendekezo haya ya sera, inatilia mkazo mwelekeo huu. Kwa mfano, hata vyama vinavyodai kuwa vya ujamaa wa kidemokrasia, kama vile Chama cha Kidemokrasia cha mrengo wa kati kushoto nchini Italia, vinatumia hoja za kupinga uhamiaji kupata viti

20. Aderanti Adepoju pamoja na Corrado Fumagalli na Nanjala Nyabola, eds., *Africa Migration Report: Challenging the Narrative [Ripoti ya Uhamiaji Afrika: Kubadilisha Mitazamo]* (Addis Ababa: International Organization for Migration [Shirika la Uhamiaji la Umoja wa Mataifa], (2020), https://publications.iom.int/system/files/pdf/africa-migration-report.pdf [https://perma.cc/CQR7-VHE7].

21. McAuliffe na Triandafyllidou, *World Migration Report 2022 [Ripoti ya Uhamiaji Duniani 2022].*

22. "Refugee Data Finder," UN High Commissioner for Refugees (statistics) ["Kitafuta Data ya Wakimbizi", Shirika la Wakimbizi la Umoja wa Mataifa (takwimu)], ilifunguliwa 3 Mei, 2022, https://www.unhcr.org/refugee-statistics/ [https://perma.cc/T2VD-K6GD].

vingi bungeni.[23] Vivyo hivyo, ingawa Chama cha Kidemokrasia cha Marekani ambacho ni cha mrengo wa kati kushoto kiliahidi kubatilisha sera nyingi za itikadi kali za utawala wa rais Trump, baadhi ya mifumo mikali iliyowekwa na rais Trump ya kudhibiti mipaka bado ingalipo, ikiwa ni pamoja na uondoaji chini ya Sehemu ya 42 inayoruhusu Mamlaka ya Ulinzi wa Mipaka kumfukuza nchini mtu yeyote "anayewasili kutoka nchi ambapo ugonjwa wa kuambukizwa ulikuwepo."[24] Kanuni hii inatumika sana kuwarudisha wanaotafuta kimbilio na wakimbizi wanaopitia nchi za Amerika ya Kati na Visiwa vya Karibi, ikiwemo Haiti.

Wahamiaji walio hatarini zaidi na wanaohitaji ulinzi zaidi mara nyingi huwa shabaha rahisi kwa sababu wanaonekana kwa urahisi. Wakimbizi na wahamiaji huwa shabaha ya kwanza ya nchi inayopambana na mzozo wake wa mamlaka makuu kwa sababu tu wapo. Matumizi yanayoongezeka ya teknolojia za ufuatiliaji na udhibiti mipakani sharti yaeleweke katika muktadha wa serikali ambazo zinazidi kuchangamkia kutekeleza sera za kitaifa kwa wakimbizi na wahamiaji ambazo hazingekubalika kutumika kwa vikundi vingine. Barani Ulaya, serikali za Denmaki ambazo ni za uliberali kwa jina zimepitisha sheria zinazowashurutisha wakimbizi kufanya kazi,[25] za kuwanyang'anya wakimbizi wanaofika mali zao,[26] na kuwalazimisha wakimbizi kurudi katika nchi ambazo bado zina vita.[27] Yote hayo, ilhali Denmaki lipokea wakimbizi 489 wapya mwakani 2021[28] na ina wakimbizi 36,023 idadi iliyopungua ikilinganishwa na idadi ya juu ya wakimbizi 73,690[29] mwakani 2016[30]. Vituo vya Australia vya

---

23. "Europe and Right-Wing Nationalism: A Country-by-Country Guide" ["Ulaya na Utaifa wa Mrengo wa Kulia: Mwongozo wa Nchi kwa Nchi"], BBC News, 13 Novemba, 2019, https://www.bbc.com/news/world-europe-36130006 [https://perma.cc/4C9A-78Q5].

24. "42 U.S. Code § 265: Suspension of Entries and Imports from Designated Places to Prevent Spread of Communicable Diseases" ["Sehemu 42 § 265 ya Sheria za Marekani: Kusimamishwa kwa Wanaoingia na Uingizaji wa Bidhaa kutoka Sehemu Zilizobainishwa ili Kuzuia Ueneaji wa Magonjwa ya Kuambukizwa"], Cornell Law School (tovuti), ilifunguliwa 3 Mei, 2022, https://www.law.cornell.edu/uscode/text/42/265 [https://perma.cc/5BPV-JPVB].

25. "Denmark Tells Some Migrants to Work for Benefits" ["Denmark Yawaambia Baadhi ya Wakimbizi Wafanye Kazi ili Wapate Manufaa ya Umma"], BBC News, 8 Septemba, 2021, https://www.bbc.com/news/world-europe-58484953 [https://perma.cc/QCJ9-XK6C].

26. "Denmark's 'Migrant Confiscation Law' Yields Little Cash" ["Sheria ya Denmark ya 'Kuwanyang'anya Wahamiaji Mali Zao' Yaleta Hela Chache Mno"], BBC News, 4 Novemba, 2016, https://www.bbc.com/news/world-europe-37871792 [https://perma.cc/432H-AZUW].

27. "Denmark: Hundreds of Refugees Must Not Be Illegally Forced Back to Syrian Warzone" ["Denmark: Mamia ya Wakimbizi Wasilazimishwe Kurudi Syria Vitani Kinyume na Sheria"], Amnesty International, 26 Aprili 2021, https://www.amnesty.org/en/latest/news/2021/04/denmark-hundreds-of-refugees-must-not-be-illegally-forced-back-to-syrian-warzone/ [https://perma.cc/CQ9H-TV8Z].

28. Michala Clante Bendixen, "How Many Refugees Are Coming to Denmark" ["Idadi ya Wakimbizi Wanaokuja Denmark"], Refugees.dk (sehemu ya Makaribisho ya Wakimbizi), ilifunguliwa 12 Julai 2022, http://refugees.dk/en/facts/numbers-and-statistics/how-many-are-coming-and-from-where/ [https://perma.cc/N3CS-6S5K].

29. "Refugee Population by Country or Territory of Asylum-Denmark" ["Idadi ya Wakimbizi kulingana na Nchi au Eneo la Kimbilio-Denmark"], Data ya UNHCR kuhusu wakimbizi kupitia tovuti ya World Bank, ilifunguliwa 12 Julai, 2022, https://data.worldbank.org/indicator/SM.POP.REFG?locations=DK [https://perma.cc/R3D2-7RDS].

30. "Minister Praises 'Low' Number of Denmark Asylum Applications in 2021" ["Waziri Asifu 'Idadi ya Chini' ya Maombi ya Wanaotafuta Kimbilio Denmark mwakani 2021"], *Local*, toleo la Denmark, 27 Januari, 2022,

kushughulikia wakimbizi vilivyo ng'ambo vipo hasa kukwepa ulinzi wa haki za binadamu ulio nchini humo.[31]

Mara nyingi, teknolojia inayotumiwa kudhibiti uhamiaji ni teknolojia ya kijela (yaani teknolojia iliyoundwa kwenye msingi wa mantiki ya jela na magereza), iliyoundwa kudhibiti mwendo na haki za wahamiaji. Vogl na Methaven (2020) wanataja jinsi serikali ya Australia inavyotumia ufuatiliaji kama sehemu ya sera zake zilizoundwa mahsusi kuzuia uhamiaji.[32] Zaidi na zaidi, wakimbizi na wahamiaji katika mataifa mbalimbali ya Magharibi wanatakiwa kuvaa vifaa vya ufuatiliaji miguuni na teknolojia nyingine zenye misingi dhahiri ya udhibiti[33]. Muungano wa Uhuru wa Raia Marekani (ACLU) unaripoti kwamba mamlaka ya mipaka ya Marekani inatumia pamoja na mbinu nyingine za kukusanya data, mfumo wa kiotomatiki wa ufuatiliaji (ATS) unaowapatia wasafiri "alama ya 'tathmini ya hatari' inayozalishwa na kompyuta, inayodumishwa kwa miaka arobaini na ambayo ni siri na haiwezi kurekebishwa."[34] Kama ilivyotajwa, mipaka ya Umoja wa Ulaya ambayo kwa muda mrefu imeitwa "Ngome ya Ulaya" inazidi kuonyesha ngome dijitali ikiwa na ndege zisizo na rubani, kamera za joto na zana za kubaini mapigo ya moyo, zote zikinuiwa kuwakamata wahamiaji wasio halali.[35]

Serikali, ikiwa ni pamoja na zile ambazo hata kuwalisha watoto wa shule ni kwa shida, zinazidi kutumia kiasi kikubwa cha pesa mipakani kuleta picha ya uongo ya kuwa na nguvu. Kwa kweli, tunatumia asasi za wakimbizi na wahamiaji kuthibitisha mamlaka makuu ya nchi, lakini matokeo yake ni kinyume.

## BUMARENGI YA CESAIRE

Katika "Uchambuzi wa Ukoloni", Aimé Césaire, ambaye ni msomi wa uondoaji wa ukoloni kutoka Martinique, anatoa hoja za kupinga dhana potofu za kikoloni zinazostahimili, kuhimiza na kulinda ukatili na dhuluma kwa misingi ya rangi.[36] Césaire anatajwa kwamba hamu ya kumkatili "Mwingine" huongeza hamu ya ukatili ndani ya

https://www.thelocal.dk/20220127/minister-praises-low-number-of-denmark-asylum-applications-in-2021/ [https://perma.cc/6GJ6-DB6S].

31. Crock, M na Ghezelbash, D 2011, 'Due process and rule of law as human rights: the high court and the "offshore" processing of asylum seekers' ['Utaratibu unaofaa na utawala wa sheria kama haki za binadamu; mahakama kuu na ushughulikiaji "wa mbali" wa wanaoomba kimbilio'], *Australian journal of administrative law [Jarida la Australia la sheria za utawala]*, juzuu la 18, nambari. 2, ukurasa 101–114.

32. Vogl, Anthea na Elyse Methven. 'Life in the Shadow Carceral State: Surveillance and Control of Refugees in Australia' ['Maisha katika Uvuli wa Nchi ya Kijela: Ufuatiliaji na Udhibiti wa Wakimbizi Nchini Australia']. *International Journal for Crime, Justice and Social Democracy [Jarida la Kimataifa la Uhalifu, Haki na Demokrasia Jamii]* 9, nambari. 4 (26 Novemba 2020): 61–75. https://doi.org/10.5204/ijcjsd.1690.

33. AP NEWS. 'ICE Issuing More Immigrant Ankle Monitors. But Do They Work?' [ICE Inazidi Kutoa Vifaa vya Miguuni vya Kufuatilia Wakimbizi. Lakini Je, Vinafanya Kazi?], 25 Agosti 2018. https://apnews.com/article/dfcdc6302e154753a526c04706df45d6 [https://perma.cc/P9JS-DD4W].

34. Popoviciu, Andrei. '"They Can See Us in the Dark": Migrants Grapple with Hi-Tech Fortress EU' ['"Wanaweza Kutuona Gizani": Wahamiaji Wapambana na Ngome ya Teknolojia Kali ya Umoja wa Ulaya'], *The Guardian*, 26 Machi 2021, sehemu ya Global development [Maendeleo duniani], https://www.theguardian.com/global-development/2021/mar/26/eu-borders-migrants-hitech-surveillance-asylum-seekers [https://perma.cc/SSV3-6DYM].

35. *Id.*

36. Aimé Césaire, *Discourse on Colonialism [Uchambuzi wa Ukoloni]* (New York: Monthly Review Press, 2000).

jamii husika, na kwamba baada ya muda, ukatili huu utatekelezwa katika jamii hiyo na hivyo kuiangamiza jamii hiyo kutoka ndani. Maonyo ya Césaire yanaonyesha athari ya tamaduni za mipakani kwa siasa za ndani za nchi za Magharibi, ambapo kustahimiliwa kwa ukatili unaofanywa ng'ambo kunaongeza nafasi ya siasa kali nchini.

Utafiti umegundua kwamba vikundi vya mrengo wa kulia havinuii hasa kuteka serikali nzima, bali tu kufanya lugha ya ubaguzi wa walio tofauti iwe kawaida na ikubalike.[37] Kwa mfano, nchini Ufaransa, chama cha Front Nationale, ambacho sasa kinaitwa Rassemblement National (Muungano wa Kitaifa), kilianza kuungwa mkono zaidi kilipobadilisha hoja zake kuu za kisiasa kutoka za kuwapinga Wayahudi zikawa za kupiga uhamiaji.[38] Baada ya kujibadilisha hivyo, chama hicho kimefika duru ya pili (yaani kimoja kati ya vyama viwili vyenye matokeo bora zaidi) katika chaguzi tatu za kitaifa zinazofuatana. Uchambuzi sawa utaonyesha matokeo kama hayo chini Australia, Marekani, Uingereza, Canada na nchi nyingine nyingi, ambapo hata vyama vya uliberali kwa jina kutumia hoja za mrengo wa kulia kuhusu uhamiaji inazidi kuwa kawaida. Jaribio hili la kutumia mpaka kusuluhisha mzozo wa mamlaka makuu lina athari mbaya ya kuendeleza mzozo huo - iwe ni msimu wa mawaziri wakuu wengi Uingereza au jaribio la tarehe 6 Januari la kupindua serikali Marekani.

Mwelekeo wa mzozo wa hali ya kuwa nchi ni kwamba hoja za ubaguzi mpakani hazifanyi nchi iwe thabiti zaidi, kwa kweli zinaidhoofisha kwa kuimarisha siasa za ukabila na utaifa, na kutumia mpaka kama chombo cha kutekeleza siasa hizi kama sera katika muktadha ambapo ni vigumu sana kupingwa. Wakimbizi na wahamiaji wapo hatarini zaidi kuathiriwa na utaratibu uliofichika wa kutunga sera, pamoja na sera za kikatili, huku wakipitia vitendo vibaya zaidi vya udhalimu wa nchi.[39] Vivyo hivyo, zaidi na zaidi, teknolojia zinazotumiwa kudhibiti uhamiaji ni zile ambazo bado zinabishwa kwa sababu za kimaadili au kimaslahi au teknolojia hizo zimekatazwa zisitumike kwa wenyeji; hali inayodhihirisha kwamba wakimbizi na wahamiaji wapo katika hatari ya ukiukaji mahususi wa haki dijitali. Hivyo, huku mamlaka ya mipaka ya Umoja wa Ulaya ikiwa imetumia angalau Yuro milioni 321 kati ya 2007 na 2022 kwa teknolojia ya kulinda mipaka, inafanya hivyo bila teknolojia madhubiti za kulinda umma barani Ulaya dhidi ya matumizi mabaya ya teknolojia kama hizo.[40]

Utamaduni wa kisasa wa mpakani barani Ulaya unazidi kujikita katika vitendo vya ubaguzi na kwa kweli, ubaguzi wa rangi; hili linadhihirika katika mwitiko unaozidi kuwa wa vurugu kwa aina zote za uhamiaji. "Fortress Europe" (tafsiri yake "Ngome Ulaya"), ni istilahi ambayo inatumika sana na waundaji sera wengi barani Ulaya kurejelea shauku

---

37. Greven, Thomas. 'The Rise of Right-Wing Populism in Europe and the United States' ['Kuibuka kwa Siasa za Mrengo wa Kulia za Kufurahisha Umma Ulaya na Marekani'. *A Comparative Perspective [Mtazamo wa Kulinganisha] - Friedrich Ebert Foundation*, 2016, 1.

38. *Id.*

39. "Manus Island: Australia Abandons Refugees to a Life of Uncertainty and Peril" ["Kisiwa cha Manus: Australia Yawaacha Wakimbizi katika Maisha ya Kukosa Uhakika na Hatari"], Amnesty International, 1 Februari, 2018, https://www.amnesty.org/en/latest/news/2018/02/manus-island-australia-abandons-refugees-to-a-life-of-uncertainty-and-peril/ [https://perma.cc/2RVR-S2TG].

40. Statewatch, 'EU Has Spent over €340 Million on Border AI Technology That New Law Fails to Regulate' [Statewatch, 'Umoja wa Ulaya umetumia zaidi ya Yuro Milioni 340 kwa Teknolojia ya Akili Unde Mipakani Ambayo Haidhibitiwi na Sheria Mpya'], Ilifunguliwa 20 Februari 2023. https://www.statewatch.org/news/2022/may/eu-has-spent-over-340-million-on-border-ai-technology-that-new-law-fails-to-regulate/ [https://perma.cc/RPJ8-LN52].

ya jumla ya kufanya mipaka ya nje isiweze kupenyeka, ingawa mipaka ya ndani ya Ulaya ni baadhi ya inayopenyeka zaidi duniani.[41] Bahari ya Kati imezingatiwa sana katika baadhi ya sera hizi, ambapo kivuko kimelindwa sana na mara kwa mara watu huachwa wafe kwa madhumuni ya kuwavunja wengine moyo. Vivyo hivi, mipaka ya ardhini katika nchi kama vile Poland, Lithuania na Hungary imeibuka kama eneo lingine tata. Vifo katika mipaka ya Ulaya havikubaliwi tu, bali pia serikali zinavichukulia kuwa maudhi ya siasa za kieneo badala ya kwa undani kama mapungufu ya kimaadili ya sera, huku idadi ya vifo hivyo ikizidi kuongezeka.[42] IOM inaitaja Bahari ya Kati kama "mpaka hatari zaidi duniani" kwa sababu watu 33,761 wamefariki wakijaribu kuivuka, ambayo ni asilimia 40 ya vifo vyote vya mipakani duniani.[43] Asilimia tisini na tisa ya wanaojaribu kuvuka Bahari ya Kati wametoka Afghanistan, Bangladesh, Eritrea, Iraq, Nigeria, Pakistan, Somalia, Sudan, Syria na Gambia.[44]

Kujaribu kusuluhisha mzozo wa mamlaka makuu ya nchi juu ya miili ya wakimbizi na wahamiaji kunasababisha vifo na ukatili usiosemeka; yaani kuacha watu wafe ili kudhihirisha suala la mamlaka makuu.

Aidha, tamaduni na hoja hizi za mipakani husambaa duniani haraka kuliko sera za kiasi cha mamlaka makuu. Nchi zinazostawi mara nyingi hushurutishwa kukubali sera zinazoeneza upeo wa teknolojia za kijela kama sehemu ya mipango ya ufadhili wa maendeleo. Ukosefu wa utafiti huru na uwezo wa kubuni sera katika nchi nyingi umeifanya vigumu kukosoa sera kama hizo ipasavyo. Hali hii inaufanya mzozo wa mamlaka makuu kama unavyoonekana mipakani suala la kimataifa linalohitaji mshikamano mkubwa wa kimataifa kusuluhisha. Kwa wasomi wanaotathmini mzozo wa utambulisho wa mamlaka makuu na athari zake, kuna hitaji linalojitokeza la kufanya kazi bila kuzingatia mipaka ya kijiografia na ya kitaaluma. Usomi wa kihakiki katika fani za teknolojia dijitali, uhamiaji, sayansi ya siasa na nyingine, unaweza kuimarisha uelewa wa kisheria wa eneo na umuhimu wa mzozo huu. Ni kazi nzito na isiyotabirika inayohitaji kuvunja kabisa nadharia msingi za nchi na mamlaka makuu, ambazo fani ya sheria wakati mwingine huwasilisha kama ukweli usiopingika, lakini ni kazi ambayo mishowe inachangia suluhisho pana zaidi.

41. Hans-Jorg Albrecht, "Fortress Europe: Controlling Illegal Immigration," *European Journal of Crime, Criminal Law and Criminal Justice* ["Ngome Ulaya: Kudhibiti Uhamiaji Usio Halali"], *European Journal of Crime, Criminal Law and Criminal Justice [Jarida la Ulaya la Uhalifu, Sheria ya Jinai na Haki Jinai]* 10, nambari 1 (2012).

42. "Thousands Protest Migrant Deaths at Spain-Morocco Border," ["Maelfu Waandamana Kulalamikia Vifo vya Wahamiaji kwenye Mpaka Kati ya Uhispania na Morocco"], Associated Press, 1 Julai, 2022, https://apnews.com/article/africa-migration-race-and-ethnicity-spain-5c69182b3d7bdaffc3418ecfe2ded1f9 [https://perma.cc/Z2FS-P76Y].

43. Harsha Walia et al., *Border and Rule: Global Migration, Capitalism, and the Rise of Racist Nationalism [Mpaka n Utawala: Uhamiaji Duniani, Ubepari na Kuibuka kwa Utaifa wa Ubaguzi wa Rangi]* (Chicago: Haymarket Books, 2021).

44. Walia et al., *Border and Rule [Mpaka na Utawala]*.